2002

QUALITY IS OUR CONCERN 002

# DARASA LA NANE

**8**

# UTABIRI THABITI - 2020

CONQUEROR

**Muda: Saa 1 Dak 40**

# KISWAHILI LUGHA

**SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO**

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Ukisha chagua jibu lolote lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala siyo katika kijitabu hiki cha maswali

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu:
   **NAMBA YAKO YA MTIHANI**
   **JINA LAKO**
   **JINA LA SHULE YAKO**
6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule, na zile namba tatu zako wewe mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.
9. Kwa kila swali 1-50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu MOJA tu kati ya hayo manne ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

*Mfano*

**21.** Kamilisha methali: Ukiona vyaelea________

A. vyaenda B. vyaundwa
C. vyazima D. vyaisha

Jibu sahihi ni B

**Katika karatasi ya majibu**

**11** [A] [B] [C] [D] **21** [A] ~~[B]~~ [C] [D] **31** [A] [B] [C] [D] **41** [A] [B] [C] [D]

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali 21, kisanduku chenye herufi B ndicho kilochochorwa kistari.

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku **kimoja tu** kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Karatasi hii ya maswali ina kurasa 7 zilizopigwa chapa.**

QUALITY IS OUR CONCERN 002

**Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi, umepewa majibu manne hapo. Jaza kila pengo kwa kuchagua jawabu lifaalo zaidi.**

Baada ya kuelezewa ___1___ ya pombe, alielewa ___2___ kuwa kinywaji hicho ___3___ hatari tu kwa ini lake bali ___4___ ubongo wake. Hapo ndipo alipoamua ___5___. Marafiki zake ambao walimshawishi kunywa pombe aliwatupilia mbali. Mwanzoni, asilimia kubwa ya wakazi pale kijijini ___6___. Hata hivyo, yeye na pombe waliishi kuwa ___7___. Naam, ___8___.

1. A. madhara B. ghadhabu C. adhabu D. mathara
2. A. tena B. fika C. asilani D. hata kidogo
3. A. hakikukuwa B. kilikuwa C. kilikua D. hakikuwa
4. A. hadi B. pia C. tangu D. lakini
5. A. kuwa joka la mdimu B. kumkata jongoo kwa meno C. kumtupa jongoo na mti wake D. kuona husuda
6. A. haikuamini B. hawakuamini C. hazikuamini D. hakikuamini
7. A. maji na mafuta B. kinu na nchi C. chanda na pete D. kiko na digali
8. A. ndugu mui heri kuwa naye B. mui huwa mwema C. cha mlevi huliwa na mgema D. kifo cha wengi ni harusi

Tumaini alipompata mhisani wa ___9___, alijikaza sana masomoni. Aliweza kuelewa, nomino za dhahania kama vile ___10___. Vilevile, ___11___ na tatizo la ukanusho, ___12___ kutafuta ___13___ na mwalimu. Juhudi ___14___ zilimsaidia kuelewa kuwa ukanusho wa **'ukuta umebomolewa'** ni ___15___.

9. A. kumfadhili masomo yake B. kuyathamini masomo yake C. kumdhamini masomo yake D. kuyadhamini masomo yake
10. A. maji, mafuta, uji B. wema, furaha, bidii C. kuimba, kula, kutembea D. vijiko, dawati, kalamu
11. A. alipokabidhiwa B. alipotwaliwa C. alipokabiliwa D. alipopokelewa
12. A. aliamua B. aliamuliwa C. aliamulia D. aliamrishwa
13. A. msaada B. kusaidia C. kusaidiwa D. kusaidiana
14. A. zako B. zangu C. yake D. zake
15. A. ukuta hujabomolewa B. ukuta haukubomolewa C. ukuta haujabomolewa D. ukuta hukubomolewa

***Kuanzia nambari 16 mpaka 30, chagua jawabu lifaalo zaidi.***

16. Chagua wingi wa;

**Wakala amekula mkunga yule mtamu.**

A. Mawakala wamekula mikunga ile mitamu.
B. Mawakala wamekula wakunga wale watamu.
C. Wakala wamekula mikunga wale watamu.
D. Mawakala wamekula mikunga wale watamu.

17. Tambua sentensi sahihi kati ya hizi.

A. Simba amemla mbuzi wote.
B. Darasani kwote kumejaa maji.
C. Kijana aliyefiwa na wazazi ana huzuni mwingi.
D. Huyu kondoo ni wa mjomba wangu.

18. Jibu lipi ambalo **halijalinganisha** nomino na ngeli zake kwa usahihi?

A. **Kipepeo** - A WA, KI - VI
B. **Moyo** - U - I, U - ZI
C. **Bustani** - I - ZI, PA - KU - MU
D. **Ua** - LI - YA, U - ZI

19. Chagua sentensi iliyotumia **'ku'** kuonyesha ukanusho.

A. Uwanjani kulikofyekwa kumejaa nyasi.
B. Kutembea kwingi ndiko kuchoka sana.
C. Mgeni hakuwasili tulivyotarajia.
D. Nilikuona ukifanya mazoezi.

20. Sentensi ipi iliyoakifishwa kwa usahihi?

A. Walinunua matunda mengi; tufaha, maembe na mananasi.
B. Bwana Musa - mwalimu wetu wa Kiswahili - ni mwalimu mzuri.
C. "Wewe ni nani"? Mwalimu aliuliza.
D. Amina amepewa zawadi: alifaulu katika mtihani.

21. Orodha ipi inayoonyesha **maagano** pekee?

A. Alamsiki, kwaheri, buriani.
B. Waambaje, chewa, cheichei.
C. Sabalheri, alamsiki, masalheri.
D. Aheri, binuru, marahaba.

22. Tambua sentensi iliyotumia **'ki'** kuonyesha wakati endelezi.

A. Ukianza kusoma kwa bidii utafaulu.
B. Mzee alikuwa akitembea polepole sana.
C. Kijibwa kilivuka barabara kilipoliona gari.
D. Kijana yule aliimba akicheza.

23. **Jua la mtikati** huwa wakati upi?

A. Macheo.
B. Alasiri.
C. Machweo.
D. Adhuhuri.

24. Tambua aina za maneno yaliyopigiwa mistari.

**Mtoto huyu anatembea <u>haraka</u>, <u>yule</u> amesimama.**

A. Kielezi, kiwakilishi
B. Kitenzi, kiashiria
C. Kielezi, kivumishi
D. Nomino, kiwakilishi

25. Neno **mwambao** lina silabi ngapi?

A. 4
B. 3
C. 7
D. 5

26. Jibu lipi lililo na kikundi cha mavazi ya kike pekee?

A. Sketi, rinda, bulibuli.
B. Bwelasuti, kocho, kizibao.
C. Shimizi, buibui, gagro.
D. Shumburere, blauzi, sidiria.

**27.** Chagua jibu lililo na kitenzi kilichoundwa kutokana na sifa.

A. Ujuzi - jua
B. Amini - mwaminifu
C. Mwalimu - funza
D. Vumilivu - vumilia

**28.** Sentensi ipi iliyotumia **tasfida**?

A. Wageni wamejaa hadi nafasi ya kutema mate haipatikani.
B. Mji ule ulimpokea kwa mikono miwili
C. Shangazi yangu amejifungua.
D. Mzee Tembo hulewa chakari kila siku

**29.** Tambua matumizi ya **'kwa'** katika sentensi.
**Naima ameenda <u>kwa</u> harusi ya mjomba.**

A. Kujibu swali.
B. Kuonyesha uhusiano.
C. Kuonyesha mahali.
D. Kuonyesha sababu.

**30.** **Tamaa** ni kwa **fisi** kama vile **maneno mengi** ni kwa

A. kasuku.
B. chiriku.
C. tai.
D. kunguru.

***<u>Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 31 hadi 40.</u>***

Yamkini wanafunzi wengi hudhani kwamba michezo ya riadha huanzia shuleni. Hata hivyo, ukichunguza kwa makini utapata kwamba watu wengi huanza kushiriki katika riadha na michezo mingine wakiwa watoto wakembe. Ikiwa unakumbuka vyema, utapata kwamba ulianza kucheza kandanda pindi tu ulipoanza kutembea. Mara ya kwanza mpira wako ulikuwa kikombe ulichotiliwa uji au nguo yako ambayo uliivua na kuichezea. Ulipokua kidogo, wewe na wenzako mliunda mpira wa karatasi, majani au vitambaa, ambavyo mara nyingi mliokota kwenye majalala.

Labda hujasahau mara yako ya kwanza kuogelea. Sitashangaa ukiniambia kuwa kidimbwi chako cha kwanza kilikuwa maji machafu yaliyokuwa nje ya nyumba yenu. Wengine wataniambia kuwa waliogelea kwenye vijito vilivyojaa konokono bila kuwa na mwao na hatari ya kuambulia magonjwa. Ama kwa kweli, **jambo usilolijua ni kama usiku wa giza**. Licha ya kuogelea, wewe na wenzako mlishiriki katika michezo mingine kama vile kurusha tiara, kibe, kuwinda ndege kwa mawe, kuvutana kwa kamba, kuruka kamba na kuzungushia tairi kwenye kiuno. Wakati mwingine mlikimbizana ili kuona **anayempiku** mwingine.

Ukiulizwa kuhusu michezo mliyoshiriki mkiwa watoto, utasema kuwa michezo hii mliitunga wenyewe. Kadhalika nyinyi wenyewe ndinyi mliotunga sheria ambazo zilidhibiti uchezaji wenu. Wale ambao walivunja sheria hizi walipewa adhabu kali kama vile kutengwa na kikundi au kupewa kazi ya kuwahudumia wengine wakiendelea kucheza. Bila shaka adhabu hizi ziliimarisha nidhamu miongoni mwenu. Kadhalika, michezo hii yenu **haikuwaleta pamoja tu bali pia ilichangia kuimarisha urafiki**. Mathalani, mmoja wenu alipoumia, kundi zima lilimshughulikia. Aidha, michezo hii ilikuza ubunifu na ujasiri. Kule kutengeneza mipira na nyavu kwa nyasi au karatasi kuliwapa stadi za kuunda hata vifaa vikubwa zaidi. Vilevile, ni wazi kwamba ulipoirusha tiara yako na kuwashinda wenzako katika mbio, ulijihisi kuwa shujaa na kujiamini zaidi. Wakati mwingine hata ulichaguliwa kuwa kiongozi wa kundi kutokana na umahiri wako katika michezo.

**Nina matumaini kama tai mtini** kuwa michezo hiyo yenu iliwasaidia kujenga misuli na kuimarisha viungo vya mwili. Ni wazi kwamba wakati uliposhiriki michezo hii ulijihisi mwepesi zaidi, na uliweza kutekeleza mengi bila kuchoka haraka. Zaidi ya hayo, michezo hiyo ilikuwezesha kupata usingizi wa pono na kuraukia shule bila kulazimishwa na mlezi wako. Ikumbukwe kwamba michezo hiyo hiyo ndiyo inayoendelezwa hata shuleni. Manufaa yake ni mengi hata kwa watu wazima. Wanaoshiriki michezo hii katika nyanja za kieneo na kimataifa hujifaa kwa mengi. Kuna wale ambao hushinda tuzo na nishani mbalimbali kutokana na weledi wao. Wengine hupata fedha nyingi na kuambulia utajiri wa ghafla. Pia baadhi huteuliwa kuchezea timu za kimataifa na kuziletea familia na nchi yao sifa kuu. Wapo wanaoajiriwa kuwa makocha na marefa wa timu za kitaifa na kimataifa.

Mti hauendi ila kwa nyenzo. Nao utendaji wako katika michezo unahitaji kuboreshwa kila mara. Ushauri wa walimu na wanajamii wengine ni muhimu katika kukuimarisha michezoni. Hao hukuelekeza kuhusu namna ya kuutumia muda wako vyema; usije ukaegemea sana katika michezo ukasahau mengine muhimu kama vile kudumisha usafi, kuzingatia masomo na mahusiano ya kifamilia. Kadhalika ni sharti ufuate nasaha ya waelekezi wako kuhusu njia bora ya kutumia pato ambalo huenda ukapata kutokana na michezo.

**31.** Aya ya kwanza imedhihirisha kuwa mwandishi;

A. ameshuhudia wanafunzi wakidhani kwamba michezo ya riadha huanzia shuleni.

B. ana uhakika kuwa wanafunzi wengi hudhani kwamba michezo ya riadha huuanzia shuleni.

C. anaonelea kwamba yawezekana wanafunzi wengi hudhani kwamba michezo ya riadha huanzia shuleni.

D. anadai kuwa yakini wanafunzi wengi hudhani kwamba michezo ya riadha huanzia shuleni.

**32.** Kulingana na aya ya kwanza, ni kweli kuwa;

A. jambo litokealo kuwa kubwa huanza mapema polepole.

B. mpira tuuonao ukiwa mkubwa ulianza ukiwa kikombe au nguo.

C. uchunguzi wa makini unawahitaji watu wengi waanze kushiriki radha wakiwa wakembe.

D. kukumbuka vyema humwezesha mtoto kuanza kucheza kandanda akiwa mdogo.

**33.** Ni kweli kwamba **jambo usilolijua ni kama usiku wa giza** kwa sababu

A. mtu huweza kuchezea konokono bila kufahamu kuwa ni hatari.

B. mwandishi aliogelea kwenye vijito vilivyojaa konokono bila kujua hatari ya kuambulia magonjwa.

C. mtu huweza kufanya jambo la kumletea hatari au madhara ikiwa hajui kuwa jambo hilo ni hatari.

D. maji yaliyoajaa konokono huweza kumdhuru mtu usiku wa giza bila kujua.

**34.** Maneno **'anayempiku'** yametumika katika kifungu kumaanisha

A. aliyemshika.

B. aliyetoshana.

C. aliyemwona.

D. aliyemshinda.

35. Ni kweli kuwa michezo ya watoto ilikuza
A. nidhamu, ubunifu, unyonyaji.
B. ujasiri, ujanja, utepetevu.
C. ubunifu, maadili, ujasiri.
D. adhabu, ubunifu, ujasiri.

36. '... michezo hii yenu **haikuwaleta pamoja tu bali pia ilichangia kuimarisha urafiki.'** Kauli hii ina maa gani?
A. Michezo ilikuza umoja na urafiki.
B. Michezo haikuwaleta wachezaji pamoja lakini iliwafanya wawe marafiki
C. Michezo iliwasaidia watoto wawe na utengano na urafiki.
D. Michezo haikuleta umoja wala urafiki.

37. Maneno **'nina matumaini kama tai mtini'** yametumia fani gani ya lugha?
A. Tashbihi.
B. Chuku.
C. Istiara.
D. Majazi.

38. Aya ya nne inafafanua umuhimu wa michezo katika kujenga;
A. siha, maadili.
B. afya, uchumi.
C. umoja, zaraa.
D. uchumi, aila.

39. Aya ya tano inadokeza kuwa
A. utendaji wako unahitaji kuboreshwa kila mara.
B. walimu na wanajamii wanashauriwa kukuimarisha.
C. ni sharti kutumia pato ambalo huenda ukapata kutokana na michezo.
D. yawezekana mtu aegemee michezo pekee na kuyasahau mambo mengine muhimu.

40. Kulingana na makala haya **si** kweli kuwa
A. michezo mingine huanzia nyumbani na kuendelezwa shuleni.
B. michezo huweza kumletea mtu utulivu wa kiakili na kimawazo.
C. wachezaji wote hupata fedha na kuambulia utajiri wa ghafla.
D. michezo humfaidi mtu binafsi, familia na nchi yake.

***<u>Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 41 mpaka 50.</u>***

Jioni hiyo nilipowasili nyumbani, nilishangaa kuuona umati wa watu ukiwa umejaa. Nyuso zao zilionyesha mseto wa furaha chungu nzima kama mchanga wa bahari na **wasiwasi wa mwasi**. Nilibaki kinywa wazi kwa mshangao maadamu hiyo haikuwa kawaida ya mambo pale petu. Pindi tu **baba alipofumwa na mvi wa manaya**, tuliishi maisha yaliyosheheni upweke na ukiwa usiomithilika. Wapo waliojitolea kusambaza uvumi kuwa baba aliangamizwa na maradhi ya UKIMWI. Hilo liliifanya jamii ituambae kama uele wa ukoma. Ilidaiwa kuwa kujihusisha na mtu ambaye jamaa yake aliugua au kuaga dunia kutokana na ugonjwa wa UKIMWI kungesababisha maambukizi kwa watu wengine.

Haukupita muda mrefu kabla ya ami yangu na dada zake kuzuka na megine. Baada ya kumhusisha mganga maarufu pale kijijini, walikuwa wamebaini kuwa mama ndiye aliyefanya mpango wa kumwangamiza baba. Eti nia na madhumuni ya mauaji hayo ilikuwa kufaidi uhondo wa mali ya baba. Lile ambalo halikubainika ni mali gani aliyotaka kufaidi kutoka katika familia iliyodhahilishwa na umaskini uliozidi mipaka. Tulinyang'anywa chochote kilichokuwa cha thamani, tukaachiwa kipande cha shamba ambalo halikuwa na rotuba. Hakuna mimea iliyonawiri shambani pale isipokuwa nyasi.

Jioni hiyo, nilifahamu, bila shaka kuwa jambo baya tu ndilo lililokuwa limetokea. Hili ni kwa kuwa **aghalabu mambo ya maskini huwa hayafaulu**. Ghafla macho yangu yalitua kwenye mashangingi mawili yaliyokuwa yameegeshwa chini ya mti mmoja uliopukutisha majani yake. Nambari za usajili za magari hayo zilibaini kwamba yalikuwa ya serikali. Si walisema wajuao kusema kuwa mwenye macho haambiwi tazama? Karibu na magari hayo, nilimwona mama akiwa amesimama mbele ya majanadume manne yaliyovaa suti nyeusi tititi.

Tofauti na ilivyokuwa desturi yake siku hiyo uso wake ulichanua kama ua la asumini kwa furaha. Makunyanzi ambayo yalijaa usoni pake hapo awali yalikuwa yameyeyuka kama barafu kwenye kikaango chenye moto. Sikuwa na budi kusonga karibu ili nibaini jambo lililokuwa likiendelea. Kumbe maafisa wale wa serikali walikuwa wamekuja kutueleza kuwa kijishamba chetu kilikuwa na dhahabu. Aisee, ukistaajabu ya Musa utaona ya Firauni. Sote tulipigwa na butwaa tusiweze kuyaamini tuliyoyasikia. Ama kwa kweli, Mola hamwachi mja wake. Mama alipewa stakabadhi ambazo alifaa kuzitia sahihi ili mipango ya kupokezwa kitita cha pesa ianze.

Kila mja aliyekuwa pale alitafuta fursa ya kumsalimia au kupiga pambaja. Wote waliotudhalilisha na kutuona kama masuo walinyenyekea na kututhamini. Baada ya maafisa wale kuondoka, sherehe ya haraka iliandaliwa. Sijui mahali ambapo vyakula vilivyopikwa vilitoka. Paliandaliwa pilau, chapati, nyama ya mbuzi, kuku na kadhalika. Akina ami na shangazi walimwomba mama msamaha na kuahidi kushirikiana nasi kama kinu na mchi. Waambao huamba, pindi yakikaza mawi huwa karibu kuisha.

**41.** Aya ya kwanza imedhihirisha kuwa;
   A. msemaji hakutarajia umati uliofaa kuwa kwao ufurahie.
   B. familia inayozungumziwa ilizoea kutengwa na kuwa pweke.
   C. baba wa msemaji aliangamia kutokana na maradhi ya UKIMWI.
   D. jamii inayozungumziwa iliujua ukweli wa ugonjwa wa UKIMWI.

**42.** Aya ya pili inaelekeza kuwa kifo cha baba wa msemaji;
   A. kilisababisha mganga afanye uchunguzi zaidi.
   B. kilisababishwa na mama wa msemaji ili ajifaidi na mali
   C. hakikujulikana vizuri chanzo chake.
   D. kilisababisha familia yake iishi maisha ya umaskini tofauti na hapo awali.

**43.** Huenda **wasiwasi wa mwasi** uliotajwa katika aya ya kwanza ulitokana na
   A. kushangaa kuuona umati wa watu pale nyumbani.
   B. kutojua hasa jambo ambalo lingetokea.
   C. kumwona msemaji akiwasili nyumbani.
   D. kifo cha baba wa mwandishi.

**44.** Chagua nahau **isiyoweza** kutoa maana ya kauli **baba alipofumwa na mvi wa manaya**.

A. Baba alipopigwa konde la nyuma.

B. Baba alipoaga dunia.

C. Baba alipoenda na ulele ngoma.

D. Baba alipoacha mkono.

**45.** Familia ya baba wa msemaji imedhihirika kuwa yenye;

A. imani, huruma, uganga.

B. bidii, wema, amani.

C. uchochezi, utu, unyenyekevu.

D. ukatili, tamaa, ushirikina.

**46.** Methali gani inayoweza kudhihirisha ukweli wa kauli kuwa **aghalabu mambo ya maskini huwa hayafaulu'**.

A. Dau la mnyonge huendeshwa na Mungu.

B. Dua la kuku halimpati mwewe.

C. Maskini akiokota husemwa kuwa kaiba.

D. Dau la mnyonge haliendi joshi.

**47.** Ufanisi uliotokea katika familia hii ulisababishwa na nini hasa?

A. Ujirani mwema.

B. Kifo cha baba yao.

C. Majaliwa ya Mungu.

D. Juhudi za serikali.

**48.** Makala haya yamebainisha kuwa mama wa msemaji;

A. aliishi maisha ya huzuni kutokana na matatizo aliyoyapitia.

B. aliadhibiwa na Mungu kwa kumuua mume wake.

C. hakuwasamehe wale ambao walimtesa hapo awali.

D. alifanya bidii maishani na kuhakikisha kuwa shamba lake limepata dhahabu.

**49.** Kulingana na aya ya mwisho, ni kweli kuwa;

A. jamii ilimthamini mhusika na mama yake baada ya kuhamasishwa na serikali.

B. ufanisi wa familia ya msemaji ndio uliofanya familia hiyo ipendwe na ndugu na majirani.

C. sherehe iliandaliwa ili kumpongeza mama wa msemaji kwa juhudi zake za kuleta mabadiliko.

D. mama wa msemaji alitumia pesa kidogo alizokuwa nazo ili kuandaa sherehe.

**50.** Funzo lipi **lisilopatikana** kutokana na kifungu hiki?

A. Mungu huweza kumfanikisha binadamu yeyote.

B. Hatufai kuwadharau wenzetu hata kama ni dhaifu.

C. Kila jambo, hata liwe gumu, lina mwisho wake.

D. Kila shamba lina dhahabu, hata liwe la maskini.